## TANGAZO LA UMMA

## KONGAMANO LA UNUNUZI WA UMMA, 2026
## KUONGEZWA KWA MUDA WA KUJISAJILI

Taasisi Nunuzi, Wazabuni, Wakandarasi, Watoa Huduma, Taasisi za Elimu ya Juu, Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs), Sekta Binafsi na wadau wengine mnajulishwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeongeza muda wa kujisajili katika Kongamano la ununuzi wa Umma la Mwaka, 2026, ***mpaka tarehe 26 Julai, 2026.***

Kongamano hii linalenga kuwakutanisha wataalamu wa ununuzi kutoka sekta ya umma na binafsi pamoja na wadau wengine wa ununuzi ili kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu bora za utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa umma Nchini.

| | |
|---|---|
| **Kaulimbiu ya Kongamano:** | **"Kutumia fursa ya Ununuzi wa Umma Kidijitali kufikia Uchumi Endelevu, Shirikishi na Shindani kuelekea Dira 2050"** |
| **Tarehe za Kongamano:** | **29 Julai** hadi **31 Julai, 2026**. |
| **Mahali:** | Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) |
| **Usajili:** | Usajili wa washiriki utafanyika kupitia tovuti: https://tsms.ppra.go.tz/ Usajili utakamilika baada ya malipo ya ada husika kuthibitishwa. |
| **Mwisho wa Usajili:** | **26 Julai, 2026.** Hakutakuwa na usajili wakati wa tukio. |
| **Mawasiliano:** | Wakili Fikiri O. Ngakonda, Barua pepe: fikiri.ngakonda@ppra.go.tz, Simu: 0714 928 154. |

Asanteni kwa ushirikiano wenu

*Mha.* A. J. Suluo
**Kny: MKURUGENZI MKUU**

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)